

# Uchunguzi wa COVID-19 kwa kutumia POCT ya Haraka

Vifaa vya POCT ya Haraka vya kupima COVID-19 vinaweza kutumiwa nyumbani.

Majibu ya POCT yanaakisi hali ya mtu kwa wakati huo tu.

POCT ya COVID-19 ni madhubuti zaidi ikitumika mara kwa mara, ikiwezekana mara 2 au 3 kwa wiki.

Ikiwa una dalili za COVID-19, unapaswa kufanya kipimo cha PCR cha maabara katika kituo cha upimaji, bila kujali majibu yako ya kipimo cha haraka kwa kutembelea [gnb.ca/gettestedcovid19](https://gnb.ca/gettestedcovid19) au kupiga 811.

## VIFAA VYAKO VYA KUPIMIA NI PAMOJA NA:




**Pamba ya kuingiza puani**



**Kichupa cha kupimia**



**Maji maji ya kusawazisha asidi**



**Stendi ya kichupa**



**Katriji ya kupimia**

## UTAHITAJI:


- Kiambaza safi, tambarare
- Kitakasa mikono
- Kipima muda au saa

## KABLA HUJAANZA

- Hakikisha nyenzo zote za kupimia zina joto la chumba (18-30°C) kabla ya kuzitumia. Nawa mikono yako
- Safisha kiambaza cha kupimia
- Fungua vifaa vyako vya kupimia Toa katriji ya
- kupimia kwenye mfuko
- Andika jina lako kwenye katriji ikiwa mnapima zaidi ya mtu mmoja




**Kutazama video ya maelekezo**



Kipimo cha haraka cha BTNX


## HATUA YA 1

- Weka kichupa cha mkusanyiko katika stendi ya kichupa ili iwe wima.
- Weka majimaji yote ya kusawazisha asidi ya matumizi ya mara 1 kwenye kichupa cha kupimia.




## HATUA YA 2

- Ingiza pamba kwenye tundu la pua, kwa takribani sentimita 2.
- Sugua na zungusha pamba hiyo mara 10 na rudia kwenye tundu lingine la pua kwa kutumia pamba hio hio.




## HATUA YA 3

- Zamisha ncha ya pamba kwenye majimaji ya kwenye kichupa cha kupimia, ukigeuza na kuzungusha pamba kwa sekunde 10.
- Kamua pamba mara 10-15 kwa kuminya kichupa na pamba kwa pamoja.
- Acha pamba ndani ya majimaji na iache kwa dakika 2 kwenye stendi ya kichupa.



## HATUA YA 4


- Ondoa pamba kwenye kichupa cha kupimia huku ukikamua majimaji yaliyobaki.
- Funga nozeli kwenye kichupa cha kupimia na minya matone 3 kwenye kishimo cha duara cha katriji ya kupimia.



## HATUA YA 5


- Weka kipima muda kwa dakika 15. Baada ya dakika 15, mstari wa rangi utaonekana kwenye kidirisha cha matokeo.
- Ukimaliza, tupa vifaa vya kupimia, takatisha mikono yako, na safisha eneo lako la kupimia.

## HUJAAMBUKIZWA



**Mstari moja katika alama C, hakuna mstari katika alama T.** Huitaji kutoa ripoti, endelea na ratiba yako ya upimaji.

## UMEAMBUKIZWA



**Mistari miwili: mmoja katika alama C, mmoja alama T.** Unapaswa kujitenga mara moja. Ili kufanya kipimo cha uthibitisho, tembelea [gnb.ca/gettestedcovid19](https://gnb.ca/gettestedcovid19) au piga 811.

## MAJIBU BATILI

**Majibu yako yasipoendana na mifano yoyote hapo juu ya HUJAAMBUKIZWA au UMEAMBUKIZWA, kipimo hakijafanikiwa.** Pima upya hadi upate majibu ya **umeambukizwa au hujaambukizwa**

**Ikiwa majibu yako ya Kipimo cha POCT ni UMEAMBUKIZWA tafadhali jitenge na weka miadi ya mtandaoni ya kufanya kipimo cha PCR kupitia [gnb.ca/gettestedcovid19](https://gnb.ca/gettestedcovid19) au piga 811.**